

A Wazao wa Nuhu:

❖ Laana ya Kanaani.

- Drunkenness makes us lose self-control (Proverbs 23:31-35). Noah got drunk and undressed in his tent.
- Hamu alimwona baba yake na akamcheka, yaani kumvunjia heshima, na akavunja amri ya tano. Na akawaeleza ndugu zake wengine. Kanaani mtoto wa Hamu yawezekana alikuwa naye wakati huo (Mwz. 9:22).
- Laana ya Kanaani ilihukumu matendo yote maovu ya uzao wake. Pia iliutambulisha uzao wa Shemu kama mkombozi wa mataifa yote (Mwz. 9:25-27; 22:18).

❖ Historia ya mataifa.

- Mwanzo inataja vizazi 70 vya Nuhu. Kila ukoo ulikaa katika maeneo tofauti. Matokeo yake kukawa ni mataifa 70 duniani.
- Wote walijua juu ya kisa cha dhambi na ahadi ya ukombozi ambayo Nuhu alikuwa amewahubiria. Adamu alikuwa ameshamwambia Lameki, na Lameki akamwambia Nuhu mwanae.
- Cha ajabu, watu wachahe tu wakabakia kuwa waaminifu kwa Mungu.

B Mnara wa Babeli:

❖ Uasi.

- Kusanyiko la Babeli lilikuwa ni uasi wa wazi dhidi ya Mungu.
- Babeli inawakilisha kila vuguvugu linalotaka kuchukua nafasi ya Mungu, likitiwa nguvu na Shetani pamoja na falsafa yake (Is. 14:14; Uf. 18:2).

❖ Mungu alishuka.

- Mungu hakusubiri wanadamu wamfikie (jambo ambalo hata hivyo haliwezekani). Alishuka Mwenyewe.
- Mungu alishuka kabla uasi haujafika mbali sana. Aliwazuia wanadamu kutoka katika kujiharibu wenyewe tena (Mwz. 7-8).
- Kwa namna ile ile, Mungu alishuka “Hata ulipowadia utimilifu wa wakati” (Gal 4:4) wa Yesu kutuweka huru kutoka katika uharibifu na kutupatia uzima wa milele.
- Hatuwezi kumfikia Mungu, kwahiyo Alishuka chini kwa neema Yake.

❖ Kutawanyika.

- Wanadamu walijaribu kujijengea lango hadi kwenye kiti cha enzi cha Mungu ili wakinyakue, lakini ikawa sehemu ya machafuko [“Babeli” humaniasha “lango la Mungu” katika lugha ya Akkadian, na linafana na kitenzi cha kiebrania “kuchanganya”].
- Pale wanadamu walipotoka safinani, waliagizwa kuijaza dunia (Mwz. 9:1), lakini walikataa kufanya hivyo. Baada ya Babeli walilazimishwa kutimiza agizo.
- Baadhi yao bado waliendelea kumkataa Mungu, waliabudu sanamu, na hatimaye kupote.
- Hata hivyo, masalia walibaki kuwa waaminifu na kuendelea kumwabudu Mungu (Mwz. 11:27). Mungu pia anao masalia waaminifu leo.